


Ofisa Mifugo Kata ya Bulige, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, Dk. David Sospiter, akimchoma punda sindano ya kumkinga na magonjwa ya ngozi na minyoo katika viwanja vya Shule ya Msingi Segese kwa ufadhili wa Shirika lisilo la Kiserikali la Kutetea Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO). **PICHA: SHABAN NJIA**

Scanned by CamScanner

**...fa kilianza na wanachama 73, hivi sasa wamebaki watatu**

# Mpina avunja mkataba wa kituo cha ukuzaji samaki

**Na MICHAEL KATONA,** *Ruvuma*

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imevunja mkataba kati ya kituo cha ukuzaji wa samaki cha Ruwila, Wilaya ya Songea Mjini na wawekezaji wa kikundi cha Sofa, kilichokuwa kinaendesha kituo hicho, baada ya mwekezaji kushindwa kufikia malengo ya mkataba huo.

Akitangaza uamuzi huo mwishoni mwa wiki iliyopita mkoani hapa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliyetembelea kituo hicho, alisema amegundua kuwa kinaendeshwa kwa hasara kwa miaka kumi tangu mwaka 2010.

Shughuli za ufugaji wa samaki kwenye mabwawa yaliyopo ndani ya kituo hicho, zilikuwa zikiendelezwa na wanachama wastaafu wa kikundi cha Sofa, ambao wakati wanaanza, walikuwa 73, lakini mpaka sasa wamebaki watatu.

Waziri Mpina alisema serikali ya awamu ya tano inaendelea na mkakati wa kuwawezesha wananchi, hususan wajasiriamali, waweze kuinua uchumi wao kupitia ufugaji wa samaki, kwa kutengeneza mabwawa kwenye maeneo wanakotoka ili hatimaye wawe wazalishaji wa samaki.

Alisema lengo la serikali kwa sasa ni kumsaidia mwananchi aweze kunufaika na rasilimali za samaki kwa kufuga samaki kupitia vifaranga vinavyopatikana kwenye vituo vinavyosimamiwa na serikali.

"Kutokana na hali ya uendeshaji wa mabwawa haya ya serikali, kumekuwa na mwingiliano sana huku kukiwa kunafanyika shughuli binafsi na za serikali. Hivyo, unaweza kufanyika wizi na ikawa ni changamoto, hata huwezi kujua, sasa mashamba haya yote hayana uangalizi wowote, kwa hiyo usimamizi wa namna hii kwa vyovyote vile utaleta changamoto.

"Kwa hiyo, Katibu Mkuu nakuagiza sasa uvunje mkataba huu mara moja na Sofa na kama Sofa wanahitaji kupata msaada kutoka kwenye wizara kusaidiwa kule watakapokwenda kuchimba mabwawa, hatutasita kufanya hivyo," alisema.

Alitaka Sofa wasikatishwe tamaa kwa kuwa tayari walishaanzisha hatua ya ufugaji wa samaki kwenye kituo hicho na Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mjini iwasaidie kupata eneo lingine kwa ajili ya kutengeneza mabwawa yao.

Alisema mabwawa ya sasa yaliyopo, ambayo ni matatu, kila wanapovuna samaki wanayaachia, wasinyang'anywe.

Mkurugenzi wa ukuzaji viumbe maji, Dk Nazael Madala na Mwanasheria wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Shigi Magesa, kwa nyakati tofauti walisema kumekuwepo na ukiukwaji wa mkataba wa uendelezaji wa ufugaji wa samaki katika kituo hicho.

Dk. Madala alisema kihistoria, Sofa walikuwepo kwenye uendelezaji wa ufugaji wa vifaranga vya samaki wakati idara ilikuwa haijaanza, lakini shughuli zake zilikuwa sio nzuri za uendelezaji na ufugaji wa samaki.

"Kama mtu hajafuata matakwa ya makubaliano yaliyoingiwa, inatakiwa waweze kushughulikiwa au wanatakiwa wawajibishwe kwa kutofuata makubaliano kama mkataba unavyosema," alisema Magesa.

Kiongozi wa Ushirika wa Sofa, John Jonathani, akielezea sababu za kushindwa kufikia malengo ya ufugaji wa samaki kama ambavyo walikubaliana, alisema wastaafu walioanzisha walikuwa 73, lakini kwa kipindi kirefu hawakuweza kuusimamia mradi huo na ilipofika mwaka 2015, wastaafu wachache waliokuwa wamebaki walishauriwa na uongozi wa mkoa kama wengi wamekufa au wameshindwa, waongeze nguvu kwa kushirikiana na wananchi wengine katika utaratibu wa PPP.

## ARDHI

Scanned by CamScanner

JIONGEZE
MTANZANIA

# TUMIA VIZIMBA UFUGE SAMAKI WENGI KATIKA ENEO DOGO





"Kwenye bwawa moja la mita tatu wanakaa vifaranga 100 hadi 160 na bwawa la mita mbili wanakaa samaki wakubwa wanne hadi 10, wakati kwa upande wa ufugaji wa vizimba, kizimba kimoja cha mita tisa kwa nne inaweza kufuga samaki 9,000 hadi 12,000."

MAMBO MUHIMU



JIACHIE NA MAMA
# KILIMO

S&J 0 782 910 002

## Bata mzinga anahitaji chakula cha kutosha



DILI ZA TOWN: SABABU ASALI YA NYUKI WADOGO KUUZWA GHALI UK 4

Scanned by CamScanner

# Watoto wanaovua samaki makorongoni waonywa

NA DANSON KAIJAGE, CHAMWINO.

WAZAZI wanaoishi karibu na makorongo yanayotiririsha maji kutoka bwawani wametakiwa kuwa makini na watoto wao ambao wamekuwa wakienda makorongoni huko kwa lengo la kuvua samaki kambare.

Ushauri huo ulitolewa na Diwani wa Viti Maalum wa Kata ya Iloje, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Hilda Kadunda (CCM) alipozugumzia madhara yanayoweza kujitokeza iwapo wazazi hawatakuwa makini na watoto wao.

Alisema kwa kipindi ambacho mvua inaendelea kunyesha, maji mengi yanatoka katika Bwawa la mtera na kuingia kwenye makorongo mbalimbali na maji hayo yanasafiri na samaki aina ya kambare ambapo jamii kubwa hupenda kutumia fursa hiyo kuvua samaki kwa lengo la kujipatia kitoweo na wakati mwingine kujiongezea kipato.

Kipindi kama hicho cha kuvua samaki hao hujulikana "mtaji rungu" kwa maana ya kila mmoja anaweza kumvua samaki kambare kwa kutumia rungu kumpiga kichwani huku watoto wakilazimika kuingia kwenye maji yanayotembea.

"Wakati wa kipindi cha mvua kama hiki maji mengi hutoka bwawani na kuingia katika makorongo, maji hayo huwa na samaki wengi aina ya kambare, jamii ya huku kwa kuwa ni wavuvi hutumia fursa hiyo kuingia kwenye makorongo kwa kutumia rungu kwa ajili ya kuvua samaki hao.

"Samaki hao hsaidia jamii kupata mboga na wakati mwingine kupata samaki wengi ambao wanawaingizia kipato"alisema diwani huyo.

# Wizara kusambaza dawa za mifugo mikoa 25

Na Mwandishi Maalumu, Lindi

[illegible]

Scanned by CamScanner